# Kuongoza kwa Jumuiya: Matokeo Muhimu

*Tathmini ya Afya na Mpango wa Uboreshaji wa Afya wa Jimbo la New Hampshire*

Tathmini ya Afya ya Jimbo ilifanywa kuwa thabiti zaidi kwa kurekebisha mikakati ya ushiriki ili kukusanya uzoefu wa wahojiwa 335 wa utafiti, washiriki 28 wa kikao cha kusikiliza, na mashirika 13 yanayowakilisha vitambulisho vifuatavyo:

- Watu weusi, wenyeji, na watu wa rangi
- Wamarekani wapya (wanaojitambulisha kama mkimbizi au mhamiaji)
- Viziwi na wasiosikia vizuri
- Familia zilizoathiriwa na kifungo Wafungwa
- Watu ambao ni LGBTQIA+
- Wanaokabiliwa na ukosefu wa usalama wa makazi


## Shukrani

Shukrani kwa hao wanajamii wengi walioshiriki katika kazi hii, washirika waliotuunganisha na jamii hizi, na wawezeshaji wa jamii ambao waliunda nafasi nzuri ili majirani waweze kusimulia uzoefu wao. Shukrani za ziada zinatolewa kwa Chuo cha Madaktari wa Familia cha NH na Dartmouth Health kwa utoaji wao wa motisha kwa wanajamii na mashirika yaliyochangia kazi hii muhimu.


## USULI

Katika majira ya kuchipua ya 2022, Baraza la Ushauri la Tathmini ya Afya na Mpango wa Uboreshaji wa Afya wa Jimbo la NH (Baraza) lilijishughulisha na ufikiaji wa kina kwa jamii kadhaa katika Jimbo la Granite. Baraza lililenga kuinua uzoefu wa jamii ambazo zimekuwa na uwakilishi mdogo na uhaba wa rasilimali kihistoria ili Tathmini ya Afya ya Jimbo ya 2022 ionyeshe taswira sahihi zaidi ya afya na ustawi kote NH.


Kazi hii iliongozwa na wanachama wa Kamati Ndogo ya Baraza la Ushirikiano wa Jumuiya, na kuwezeshwa na Taasisi ya Afya ya Jumuiya/JSI kwa ushirikiano na Palabras Consulting na wanajumuiya kadhaa waliotenda kama wawezeshaji. ((Nembo ya CHI/JSI + Palabras))

## MFUMO

Muhtasari wa data ufuatao unaangazia matokeo muhimu kutoka kwa kazi hii. Kila muhtasari wa data unajumuisha mandhari mahususi ya jumuiya, pamoja na uzoefu mwingine wa ulimwengu wote unaoshirikiwa na wakazi wengi wa Jimbo la Granite, bila kujali jumuiya au utambulisho wao mahususi. Kwa kuzingatia athari za muunganisho kwenye uzoefu wa mtu yeyote, na sampuli ya kipekee ya data ndani ya kila jumuiya, data kwa ujumla huripotiwa kwa jumla pamoja na baadhi ya marejeleo mahususi ya jumuiya. Matokeo mahususi ya jumuiya yameangaziwa ili kuonyesha changamoto kubwa zinazowakabili wakazi wa Jimbo la Granite katika kufikia afya na ustawi wao bora zaidi.

**"Kwangu mimi, afya njema na uzima humaanisha kuwa una maisha yasiyo na magonjwa na yasiyo na dhiki na huzuni. Ukiwa na maisha kama hayo, yanakuruhusu kuwa na maisha bora katika suala la kufanya kile unachotaka kufanya na kufikia kile unachotaka kufikia."**

NH LIVES WELL



# Mifumo ya Huduma Inayojumuisha Utamaduni

## Kuongoza kwa Jamii: Matokeo Muhimu

*Kutoka kwa Utafiti:*

- **Bima ya afya** na huduma za **afya ya akili** zilikuwa huduma za kawaida zaidi *zinazohitajika* au *kutumika* na pia huduma za kawaida zaidi ambapo wahojiwa waliripoti *vikwazo vya matumizi*.
- **Gharama ya huduma** iliwasilisha kikwazo kikubwa katika upatikanaji wa huduma katika jamii.

Katika Utafiti wa Ushirikiano wa Jumuiya wa Mwaka 2022, afya ya mwili na akili ndiyo sehemu muhimu zaidi za ustawi zilizotambuliwa na wanajumuiya. Katika utafiti huu, wahojiwa kutoka kwa jamii zinazohusika katika kazi hii waliripoti kwamba walikuwa na ugumu zaidi wa kupata bima ya afya na huduma za afya ya akili.

Vizuizi vingi vya kupata huduma ambavyo viliripotiwa na wanajumuiya waliohusika katika kazi hii vilikuwa sawa na vile vinavyokabiliwa na wakazi wa Jimbo la Granite kwa ujumla – kama vile gharama kubwa za huduma, ukosefu wa watoa huduma. Hata hivyo, wanajumuiya wengi hubeba mzigo wa ziada wa vikwazo ambavyo vinaweza kuhusishwa moja kwa moja na kipande cha utambulisho wao.

Mwanajamii mmoja **anayezungumza Kireno** aliomba rufaa kwa huduma za afya ya akili kutoka kwa daktari wake wa huduma ya msingi, lakini alipewa maagizo ya dawa na hakupewa rufaa ya ushauri au usaidizi mwingine. Hakukuwa na mkalimani katika ziara hiyo, kwa hivyo mwanajamii huyo hakuhisi kwamba mtoa huduma alichukua muda wa kusikiliza kwa dhati matatizo yake, au kufanya jitihada za kuziba pengo la lugha na utamaduni. Badala yake mtu huyu alichagua kurudi katika nchi yake ya asili kwa ajili ya huduma za afya ya akili.

## UPATIKANAJI WA MAWASILIANO

Wanajumuiya ambao hawazungumzi Kiingereza kama lugha ya kwanza waliunganisha kwa kiasi kikubwa uzoefu wao katika kupata huduma na jinsi walivyoweza kuelewa na kuwasiliana na watoa huduma. Wengi wa wanajumuiya waliozungumza kuhusu vizuizi vya lugha walieleza kuwa ukosefu wa maelezo na huduma zinazopatikana katika lugha wanayopendelea uliathiri vibaya ubora wa uzoefu na huduma.

- Kuratibu wakalimani huongeza muda na utata katika kupata huduma
- Wafanyakazi wa dawati la mbele na wa mapokezi huenda wasijue sikuzote kuhusu usaidizi wa lugha unaopatikana
- Uzoefu wa mgonjwa unaweza kuathiriwa sana na mkalimani anayepatikana wakati wa mkutano
- Utafsiri wa moja kwa moja wa maandishi kutoka kwa Kiingereza hadi lugha zingine unaweza kupoteza muktadha muhimu

## HUDUMA ILIYO SALAMA, INAYOHESHIMU UTAMBULISHO WA KIJINSIA WA MTU

Wanajumuiya wengi pia walikuwa na uzoefu sawa wa kutohisi wakiwa salama katika kupata huduma bora, ambayo ni mahususi kwa tamaduni kwa sababu mbalimbali. Mada kuu zinazoshirikiwa kuhusu uzoefu huu, zilizoangaziwa hapa chini, mara nyingi huchochewa na woga unaotokana na unyanyapaa, na pia uwezo wa watoa huduma kutoa huduma inayofaa.

***Unyanyapaa***

- Hali ya uhamiaji na hofu ya watekelezaji wa sheria huzuia watu kupata huduma
- Mapato na hali ya bima hufanya iwe vigumu zaidi kupata watoa huduma; watu wana uwezekano mdogo wa kutafuta huduma
- Watu wasiojibainisha kwa jinsia wanatambulika kwa njia isiyo sawa katika mifumo mbalimbali, na hivyo kuchangia hali ya kutengwa.

***Huduma Inayofaa Kiutamaduni***

- Watoa huduma wengi wana mafunzo duni ya desturi na kanuni za afya ya akili za tamaduni kutoka nje ya Marekani.
- Idadi isiyotosha ya watoa huduma waliofunzwa kutoa huduma ambayo inaheshimu utambulisho wa kijinsia wa mtu.

*Kutoka kwa Utafiti:* Walipoulizwa kuorodhesha maeneo ya afya ambayo yalikuwa muhimu zaidi kwao, viwango vya wastani vilikuwa:

1. Afya ya Mwili
2. Afya ya Akili
3. Ustawi wa Kihisia
4. Ustawi wa Kiroho
5. Ustawi wa Kijamii

NH LIVES WELL



# Suala la Jamii na Kuwa Sehemu ya Jamii

## Kuongoza kwa Jamii: Matokeo Muhimu

Wanajumuiya mara kwa mara walitaja watu wanaowazunguka na jamii zao kama sehemu muhimu za ustawi wao. Pia walisisitiza thamani ya kuwa sehemu ya jamii na thamani ya jumuiya.

Katika jamii zote na vyanzo vya data, mada zifuatazo ziliibuka:

- Jamii na uhusiano wa kijumuiya ni muhimu ili kufikia ustawi
- Usaidizi kutoka kwa marika huboresha ustawi
- Afya ya familia yako huathiri afya yako
- Kusuluhisha matatizo baina ya watu huongeza hali ya ustawi

*“Tunahitaji kuzungumza zaidi na kusaidia lakini wakati mwingine hatuna uhusiano wa karibu na hivyo tunapoteza fursa.”*

*“Tuna ufikiaji wa kanisa pekee – ninataka ufikiaji zaidi wa vitu vingine katika jamii.”*

## HESHIMA NA KUWA SEHEMU YA JUMUIYA

Kwa wanajumuiya wengi, “kuwa sehemu ya jamii” kunamaanisha kukubalika kabisa na kukaribishwa na jumuiya yao, bila ubaguzi. Wanajumuiya wengi – hasa watu ambao ni LGBTQIA+, wahamiaji, na wakimbizi – wanakabiliwa na uzoefu ambao unazuia hisia zao za kuwa sehemu ya jamii. Baadhi ya mambo yanayofanana katika uzoefu huu ni pamoja na:

- Kutokuwa na uwezo wa kupata usaidizi wa kutosha wakati wa mabadiliko ya kitamaduni au utambulisho
- Kutokuwa na uwezo wa kuwa wazi kuhusu utambulisho wao wote kwa kuogopa ubaguzi
- Ugumu wa kupata maeneo ya kutosha ya kuungana na watu walio na uzoefu sawa na wao
- Kutamani watetezi zaidi wanaoonekana

## KUJENGA JUMUIYA

Tafakari za wanajumuiya kuhusu kuwa sehemu ya jamii na heshima zinaonyesha pia umuhimu wa kuunda fursa za kuimarisha uhusiano ndani ya jamii (za kitamaduni na kijiografia), na katika jamii zote. Wanajumuiya katika vikundi vyote walionyesha hamu ya mahusiano zaidi ili kusaidia kujenga maelewano na fadhili baina yao.

Vile vile, wanajumuiya wengi walielezea kufadhaika kwamba uzoefu wao hauzingatiwi kila wakati au sauti zao hazisikiki wakati wa juhudi za kufanya maboresho katika jimbo lote. Hisia hii ya “kutoonekana” huzuia hisia za wanajumuiya wengi za uhusiano na jumuiya, ambayo inaweza kuchangia hatari kubwa ya kujitenga na afya mbaya ya akili.

NH LIVES WELL

# Njia za Kupata Fursa

## Kuongoza kwa Jamii: Matokeo Muhimu

Njia za kupata Fursa (Pathways to Opportunity) inaeleza baadhi ya mambo muhimu yanayoruhusu wanajumuiya kufikia ustawi wao bora zaidi wa kiakili, kimwili, kijamii, kiroho, na kihisia. Mambo muhimu yaliyochaguliwa hapa ili kuonyesha kiwango cha upatikanaji wa fursa ambayo wanajumuiya wanayo ni: Uthabiti wa Kiuchumi, Uthabiti wa Makazi, Elimu, na Usalama wa Chakula.

*Kutoka kwa Utafiti:*
Wahojiwa wanaokabiliwa na ukosefu wa usalama wa makazi walipinga vikali kwamba eneo lao lilikuwa na makazi mazuri yanayopatikana. *"Eneo langu lina makazi mazuri yanayopatikana"* pia ilikuwa na kiwango cha chini cha makubaliano katika jamii zote.

## ELIMU

Wanajamii walieleza mahitaji mbalimbali yanayohusiana na elimu. Baadhi ya mahitaji muhimu ni pamoja na:

- Usaidizi wa mawasiliano unaofikiwa kwa urahisi zaidi ili wazazi waweze kutumia mfumo vizuri zaidi na kuwasaidia watoto wao. (mf., uchunguzi wa maendeleo, mipango na nyenzo maalum za elimu, usaidizi wa kazi ya nyumbani)
- Kuongezeka kwa hali ya usalama na ulinzi kwa watoto shuleni.
- Nyenzo zaidi za maendeleo ya kijamii na kihisia, ikijumuisha fursa za ushauri.

## UTHABITI WA KIUCHUMI

Kwa kiasi kikubwa, wanajumuiya waliona kuwa ingawa wanajua jinsi wanavyoweza kuboresha afya na ustawi wao, gharama inasalia kuwa kizuizi kikuu katika njia nyingi za kufikia afya na ustawi. Uzoefu wa kawaida ulioshirikiwa katika vikundi vya jumuiya ambao unaathiri uthabiti wao wa kiuchumi ulikuwa:

- Programu zinazotoa usaidizi wa kifedha hazina rasilimali za kutosha na ni ngumu kutumia
- Fursa za ajira zinazuiwa na vizuizi vya lugha kwa wale ambao hawazungumzi Kiingereza kama lugha yao ya kwanza.

## UTHABITI WA MAKAZI

Wanajumuiya walishiriki hitaji la makazi ambayo ni salama na ya bei nafuu. Ingawa kuna baadhi ya usaidizi unaopatikana kupitia programu za hisani na zingine zinazofadhiliwa na serikali, rasilimali hizo mara nyingi hazitoshelezi kukabiliana na changamoto kubwa zinazokabili baadhi ya jamii. Sawa na uzoefu ulioshirikiwa katika kupata aina nyingine za usaidizi, woga na unyanyapaa huunda vizuizi vya ziada kwa baadhi ya wanajumuiya katika kupata makazi salama na ya bei nafuu. Mifano ni pamoja na:

- Wanajumuiya ambao hawajazaliwa Marekani wanaogopa uingiliaji kati wa kisheria ikiwa hali yao itafichuliwa wakati wa ukaguzi wa maombi ya makazi.
- Nyumba za familia hukosa usalama na hazina uthabiti tena wakati wanafamilia hawakubali utambulsho wa kijinsia wa mtu fulani

Kwa kuunga mkono huduma za ukosefu wa usalama wa makazi, mshiriki mmoja alieleza kwamba shirika la hisani lilikuwa limempatia makazi salama na alihisi kuwa jamii inayomzunguka ilikuwa imefanya kazi bora zaidi ambayo wangeweza kulingana na raslilimali walizo nazo.

*"Makazi ya bei nafuu kwa watu wasio na hati... Hatuwezi kupata makazi salama kwa sababu kila mtu anataka kuona karatasi za uraia."*

## USALAMA WA CHAKULA

Jamii zilithamini sana chakula na lishe yenye afya, lakini waliona kuwa gharama kubwa ya vyakula vyenye afya, ukosefu wa taarifa na elimu ya lishe, na upungufu wa vyakula vyenye afya katika eneo lao vilikuwa vikwazo vya kula vizuri. Mchanganyiko huu tata wa changamoto ulikabiliwa zaidi na wanajumuiya ambao hawakuzaliwa Marekani, au hawazungumzi Kiingereza kama lugha ya kwanza.

*"Usipokula vyakula vyenye afya, au kupata lishe bora, basi utakuwa mgonjwa. Usipofanya shughuli zozote za kimwili kama vile michezo na mazoezi, hapo ndipo mwili wako hautafanya kazi ipasavyo."*

NH LIVES WELL